

BARTIMAYO KIPOFU

 ...?...Katika siku hizo, ombaomba, ili kupata kitu kidogo tu kutoka kwa umma, iliwabidi kuwa na kitu kidogo cha ziada. Nasi tunaona jambo hilo huko India. Njia pekee ya ombaomba, kama angalisimama tu barabarani huku amenyosha mkono wake, na kusema, “Nipe sarafu,” ama kuomba kitu fulani, alipata chochote kwa nadra.

² Lakini kama walikuwa na maskini...Huyo jamaa mmoja alikuwa na tumbili. Alinishangaza. Angeninii, maskini tumbili huyu, angempiga kwa fimbo; achukue hiyo fimbo na kumkimbiza kote mtaani, ampige. Naye angeomba; angemwona mtu fulani akiya, halafu angemfanya huyo tumbili amfukuze tena, kisha akimbie huku na kuanguka kifudufudi, na kunyosha mikono yake, akijaribu kumfanya mtu fulani ampe kitu fulani.

³ Mwingine alikuwa na nyoka swila; na, loo, vitu mbalimbali; kila kitu ambacho wangeweza kufanya, mazingaombwe kidogo, kitu tofauti, kuvutia usikivu wa mpita njia.

⁴ Nasi tunaambiwa ya kwamba Bartimayo kipofu alikuwa na njiwa wawili wadogo, nao waliwafanyia watu vitimbi vidogo. Wangerukiana.

⁵ Nao walisema kwamba usiku mmoja mke wake aliugua. Sasa, hii inaweza kuwa ni hadithi ya kubuni. Kwa hiyo, akatoka akaenda na kumwomba Mungu, kama angemponya mke wake, kwamba ange—angewachukua hao—hao njiwa aende kuwatoa sadaka kesho yake asubuhi, kwenye sinagogi. Vema, huyo mke, akapona, kwa hiyo akaenda akawatoa hao njiwa. Halafu hakuwa na kitu cha kuvutia usikivu.

⁶ Baada ya kitambo kidogo, wakasema ya kwamba msichana wake mdogo ambaye hakuwa amemwona kamwe, kwamba aliugua usiku mmoja, nao madaktari wakasema wasingeweza kumsaidia zaidi. Na kwa hiyo—kwa hiyo kile alichofanya basi, alitoka akaenda akaomba. Naye akasema, “Bwana, nina kitu kimoja tu ninachoweza kukutolea, hicho ni mwana-kondoo wangu.”

⁷ Sasa, siku hizi kipofu kwa kawaida huongozwa na mbwa. Wana mbwa, wanawafundisha, wanaowaongoza vipofu. Na katika siku hizo, badala ya kumfundisha mbwa, walimfunza mwana-kondoo; naye huyo mwana-kondoo akamwongoza kipofu.

Naye akasema, “Mwana-kondoo huyu ndiye yote niliyo nayo. Lakini kama utamwacha msichana wangu mdogo apone, ninakuahidi, Baba, ya kwamba kesho nitakupa mwana-kondoo huyu.”

⁸ Kwa hiyo, maskini msichana huyo, kesho yake asubuhi, alikuwa amepata nafuu zaidi naye akaona alikuwa anaenda kupona. Kwa hiyo, anapanda kwenda kumtoa huyo mwana-kondoo. Naye akasema, alipokuwa akienda zake akakutana na kuhani, naye kuhani akasema, “Unaenda wapi, Bartimayo kipofu?”

Akasema, “Kuhani, ninapanda kwenda hekaluni kumtoa mwana-kondoo wangu. Mungu alimponya mtoto wangu jana usiku nami nitamtoa mwana-kondoo wangu maana nilimwahidi.”

⁹ Akasema, “Bartimayo kipofu, huwezi kumtoa huyo mwana-kondoo. Mwana-kondoo huyo,” akasema, “nitakupa pesa, nawe utaenda kwa wanunuzi ukanunue mwana-kondoo, na kumtoa *huyo* mwana-kondoo, kwa sababu huwezi kumtoa mwana-kondoo *huyo*.”

Akasema, “Ee Kuhani, kamwe sikumwahidi Mungu mwana-kondoo *fulani*. Nilimwahidi mwana-kondoo *huyu*.”

¹⁰ Na mara nyingi, sikuzote tunajaribu kufanya jambo fulani. Unajua, si karama yako wala sadaka yako, ni *wewe* ambaye Mungu anataka. Unaona. Mnaona? Akasema, “Nilimwahidi nitampa mwana-kondoo *huyu*.”

Akasema, “Huwezi kumpa mwana-kondoo huyo; mwana-kondoo huyo ndiye macho yako.”

¹¹ Akasema, “Loo, kuhani wa Mungu, ikiwa Bartimayo kipofu amemwahidi Mungu, nami ninatimiza ahadi yangu, Mungu atatoa mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu.”

¹² Na hivyo ndivyo ilivyotukia. Mungu alimtoa Mwana-kondoo kwa ajili ya macho ya Bartimayo kipofu: yule Mwana-kondoo wa Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Basi Bartimayo akafumbuliwa macho kutoka kwa Mwana-kondoo aliyetolewa na Mungu.

¹³ Naye Mwana-kondoo yuyo huyo ametolewa usiku wa leo kwa ajili ya kila mtu hapa katika jengo hili: Yesu Kristo, Mwana-kondoo wa Mungu, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ametolewa usiku wa leo kwa ajili ya dhambi zako, haidhuru ni nyeusi jinsi gani; ama ametolewa kwa ajili ya ugonjwa wako, haidhuru wewe ni mgonjwa jinsi gani, ama jinsi unavyoteseka.

¹⁴ Alipokuwa hapa duniani alienda kila mahali akitenda mema. Nasi tumemwona, kwamba hakudai; kwamba Yeye hakuwa mponyaji. Alidai ya kwamba Mungu aliponya kupitia Kwake, wala hakufanya lolote lake mpaka Mungu alipomwonyesha kwa ono, kwanza, jambo la kufanya. Akasema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo

Mwana vile vile.” Na hiyo ilikuwa ndiyo huduma Yake wakati alipokuwa hapa duniani.

¹⁵ Wakati alipokuja kwenye kaburi la Lazaro... Aliposikia kwa mara ya kwanza ya kwamba Lazaro alikuwa mgonjwa, hakisikia kwa mwanadamu, alisikia kwa Mungu. Akasema, “Rafiki yetu Lazaro ni...” Ninamaanisha, alipokuwa amekufa. Alisema, “Rafiki yetu Lazaro amelala; na kwa ajili yenu ninafurahi sikuwapo; lakini ninaenda nikamwamshe.”

¹⁶ Ndipo alipokuja kaburini, Yeye alisema, “Baba, nakushukuru kwa kuwa umenisikia Mimi: lakini kwa sababu ya hawa waliosimama karibu nalilisema.” Halafu basi, kuwafanya tu wajue, kwa mfano, kwamba wanapaswa kuomba kabla hawajafanya ishara zozote, au, kutoka kwa Mungu, au kumwomba Mungu afanye mambo; bali Yeye alisema tayari alikuwa amepokea kwa Mungu yale yatakatyotukia.

¹⁷ Basi Yesu yeye yule aliyeishi katika siku hiyo, aliyepitia kwenye malango ya Yeriko, aliyemkirimia Bartimayo kipofu kuona, Yule aliyemfufua Lazaro kutoka kaburini, Yule ambaye yule mwanamke aligusa vazi Lake, Yule aliyekuwa kwenye ile—ile tanuru iliyowaka moto pamoja na wana wa Kiebrania, Yule aliyekutana na Yohana nje ya lango, Yule aliyekuwa juu ya bahari usiku ule akitembea, Yesu yeye yule aliyesemwa, katika Biblia, kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Naye amehidiwa kuwa pamoja nasi: “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao.”

¹⁸ Sasa, hiyo ni—hiyo ama ni kweli, au ni uongo. Na kama Yesu hajafufuka katika wafu, hajafufuka katika wafu, basi, bila shaka, asingeweza kufanya yale aliyoahidi kufanya. Lakini kama amefufuka katika wafu, na anadai kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye anawajibika kwa ahadi Yake ya Kiungu kutimiza Neno Lake kwa kila kizazi. Kwa kuwa Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu.” Naye anawajibika; ahadi Zake zina hatia, mpaka atakapozitimiza kwa kila kizazi.

¹⁹ Basi hoja yangu ni hii: kwamba tuna mengi yanayohusiana na uponyaji wa Kiungu, wanavyoita; lakini hilo haliondoi kwenye kilicho halisi. Wala hakuna mtu duniani anayeweza kukuponya. Mungu tayari amefanya hivyo wakati alipomtuma Yesu duniani Naye akafa pale Kalvari.

²⁰ Hakuna mtu anayeweza kukuokoa; Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hivyo; Naye tayari amefanya hivyo. Wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, Yeye alimaliza kazi za wokovu wako kwa uponyaji na—na, uponyaji wa mwili na nafsi yako pia.

²¹ Neno lile lile linatumiwa kila wakati. Mliona somo letu usiku wa leo? Yeye alisema, “Imani yako imekuokoa.” Nalo neno la Kiyunani hapo linaitwa *sozo*. Na *sozo* linatumiwa kwa

wokovu na uponyaji wa Kiungu pia. Ama umeokolewa kimwili au umeokolewa kiroho.

²² Upatanisho ule ule ulifanywa na Mtu yule yule siku ile ile: “Kwa maana alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” Na ni: ama Biblia ni kweli, au ni uongo. Wala hakuna haja ya watu katika siku hii, ama siku nyingine yoyote, kujaribu kuielezea Hiyo vinginevyo kujaribu kuficha kutokuamini kwako. Ingali ni Ahadi ya Mungu.

²³ Na kama sikuamini ya kwamba Yesu wa Nazareti, katika maandiko ya Kitabu hiki...Bila kuondosha yoyote ya hizo. Kuna ahadi nyingi ambazo huenda nisiwe na imani ya kuzitimiza, bali ni za kweli vivyo hivyo. Wala sitaki kamwe... Kama siwezi kutembea mahali alipotembea Yoshua; kama siwezi kutembea mahali Henoko alipotembea, mpaka haikumbidi kufa na akaenda tu nyumbani pamoja na Mungu alasiri moja; kama sina imani ya kufanya hivyo, hakika sitaki kumzuia mtu mwingine yeyote aliye na imani ya kufanya hivyo, ama kujaribu kuielezea vinginevyo kwa theolojia fulani. Nitatoka moja kwa moja na kukabiliana na ukweli, na kusema, “Sina hiyo imani, lakini, hata hivyo, ni Neno la Mungu. Alisema angefanya hivyo.” Ninaliamini hivyo.

²⁴ Nami ninaamini ya kwamba Yesu yeye yule aliyesimamishwa na kilio cha Bartimayo kipofu, unaweza kumsimamisha usiku wa leo. Mwanamke yule yule aliyegusa vazi Lake, Yeye angali anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Ninaamini atafanya tu kama alivyosema. Ili awe Mungu, hana budi kutimiza Neno Lake.

²⁵ Sasa, ninaweza kuwaambia jambo fulani, nami sina budi kulighairi, mara nyingi, kwa sababu mimi ni mwanadamu tu. Mchungaji wenu anaweza kuwaambia mambo, hana budi kuyaghairi. Unaweza kumwambia jirani yako mambo, ama wapendwa wako mambo, nawe huna budi kuyaghairi. Lakini Mungu hawezi kughairi Neno Lake. Hana budi kutimiza Neno Lake. Hana budi kulitimiza kusudi awe Mungu. Hawezi kughairi yale aliyosema. Hana budi kulitimiza. Anawajibika Kwalo.

²⁶ Na hiyo ndiyo sababu ilibidi Dhabihu hii kuu itolewe. Mtu mmoja afe kwa ajili ya wote, kwa sababu mtu mmoja alitenda dhambi na kuwafanya watu wote wawe katika hali ya kufa. Na mwanadamu... Unaposhughulikia dhambi, huna budi kushughulikia magonjwa kwa sababu ugonjwa ni matokeo ya dhambi. Ugonjwa ulikuja kwa dhambi.

²⁷ Na kwa hiyo, iwapo Upatanisho ni, unahusu tu imani yako binafsi katika Mungu katika kazi zilizomalizika pale Kalvari... Ambapo kila kitu tunachohitaji, tunatulia juu ya Ahadi ya Kiungu ya Mungu ya sifa takatifu za kifo Chake pale Kalvari, ni mahali ambapo tunaponywa na ambapo tunaokolewa. Hatuna budi kutegemea hizo.

28 Hakuna mtu anayeweza kukuponya kwa kusema, “Vema, nina uwezo wa kukuponya.” Mtu anaposema hivyo, amekosea.

29 Kulikuwako, katika Biblia, ambapo Mungu aliwapa watu nguvu za kuponya, nao wakashindwa nazo; na hao walikuwa ni wale Mitume. Yesu, Biblia inasema dhahiri, ya kwamba (hili ni kwenu ninyi ndugu wa Church of Christ, hili) Yesu kweli aliwapa Mitume nguvu za kuponya. Kisha yapata siku kumi baadaye, walikuwa wameshindwa vibaya sana nazo; basi walikuwa na mtu mwenye kifafa ambaye walijaribu kumtoa pepo, wala wasingeweza kufanya hivyo. Naye Yesu akasema, “Nitawavumilia hata lini? Mleteni hapa.”

Nao wakasema, “Kwa nini hatukuweza kufanya hivi?”

Akasema, “Kwa sababu ya kutokuamini kwenu.”

Kwa hiyo, mnaona, imani ni ushindi. Tunaamini Neno Lake.

30 Sasa, Yeye kamwe hakuja na kusema alitupa nguvu za kuponya, kwa sababu hatuwezi kufanya hivyo. Yesu aliwapa nguvu za kuponya kabla ya ule Upatanisho kufanywa. Lakini baada ya Upatanisho kufanywa, uponyaji ulikalimishwa milele. Sasa, imani ya mtu binafsi katika ule Upatanisho ndiyo inayoleta matokeo ya uponyaji. Amina. Natumaini mnalifahamu dhahiri. Hakuna mtu siku hizi alie na nguvu za kuponya.

31 Sasa, ninii... Mungu ameweka Kanisani, kwanza mitume, ama, hebu nitumie neno bora zaidi siku hizi, “wamishenari.” Mbona wao, wamishenari, wamewahi kudai, ama wakataka kuitwa *wamishenari* badala ya *mitume*, sijui, ni kitu kile kile hasa: “mtu aliyetumwa.” Wamishenari, mitume, manabii, waalimu, wainjilisti: karama hizi zote zimewekwa kanisani na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa na ule Mwili.

32 Kila mmoja wa hao, kama vile mhubiri anavyohubiri Neno: “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia kwa Neno.” Halafu huyo mtu mwingine, ana karama ya kufundisha, kwa hiyo anafundisha. Na kwa hilo anawaelezea watu: “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia kwa Neno.”

33 Mwingine ni nabii ama mwonaji, ambaye amechaguliwa Kiungu kuona maono, na kutabiri mambo, na kubashiri mambo. Mtu huyo anaweza... hawezi kuponya, anaweza tu kutabiri. Lakini yote yanafanya nini? Huonyesha ya kwamba Yesu Kristo amefufuka katika wafu. Hiyo ni kweli. Naye yuko pamoja nasi leo.

34 Sasa, na kama tutadumu katika ofisi zetu, na kufanya yale Mungu atuambiyayo, wala tusiangalie kulia wala kushoto, bali tuangalie mbele huko Kalvari, Mungu atatufanyia miujiza. Nasi tuko katika siku hiyo. Hakika tunatarajia na tunajua, na tunaolewa wenyewe, kwamba ulokole kama huo umefunganishwa pande zote mbili, kwa ajili ya uponyaji wa

nafsi yako na uponyaji wa mwili wako. Lakini hata hivyo, Yesu Kristo amefufuka katika wafu na huonyesha kazi zile zile na ishara zile zile alizofanya alipokuwa hapa duniani.

³⁵ Wala kamwe hakutakuwako, kamwe hakujakuwako ama hakutakuwako na wakati ambapo mwanadamu anaweza, bila mpangilio, kufanya lolote atakalo. Yesu Kristo asingeweza kufanya hivyo, Mwenyewe. Wala hakuna mtu duniani, ama atakayepata kuwako, ambaye ataishi zaidi ya Maisha ya Bwana Yesu Kristo, maana Yeye alikuwa Mwana mkamilifu wa Mungu na Dhabihu kamilifu. Naye alisema dhahiri, ya kwamba, Yeye Mwenyewe asingeweza kufanya lolote, tena na tena, wakati baada ya wakati. Yeye alisema, “Sifanyi neno kwa nafsi Yangu, wala siwezi kufanya neno kwa nafsi Yangu, bali lile nimwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile. Mimi hutenda... Baba Yangu anatenda kazi, nami ninatenda kazi hata sasa. Sifanyi lolote mpaka Yeye aniambie, ama Yeye anionyeshe.” Kasema, “Na hukumu Yangu ni ya kweli: kwa sababu si Mimi ninayetenda jambo hilo, ni Baba Yangu. Mimi na Baba Yangu ni Mmoja.” Bila shaka.

³⁶ Wakati aliponena, ilikuwa ni sawa na Mungu akinena, kwa sababu Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Na usiku wa leo, kama mtu kweli ametiwa mafuta na Roho wa Mungu, akihubiri Neno, ni kitu kile kile kama vile Mungu akienda na Neno Lake Mwenyewe.

³⁷ Kama mtu ni mwonaji, ama nabii, na aweze kumwambia mtu binafsi jambo tofauti, ama kitu fulani cha kuwasaidia, na kama wakiona hiyo ni kweli, basi huyo ni Mungu anayenena kwa njia nyingine. Na kama yale mtu huyo asemayo hayatumiki, hayalingani na Biblia, basi mtu huyo amekosea. Lakini kama yanalingana na Biblia, ni Neno la Mungu kwa mtu huyo. Mnaelewa?

Yesu Kristo na awabariki, watu wangu. Nawapenda.

³⁸ Hatujui ni siku gani tutaitwa tuondoke katika ulimwengu huu, kila mmoja wetu. Ndipo utakapoondoka, ama kama nikitangulia, ama ukienda, kuna jambo moja la hakika tujualo, ya kwamba mtu amewekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu. Nasi hatuna budi kusimama katika Uwepo Wake kwenye Siku hiyo. Sina budi kusimama mbele yenu, hamna budi kusimama mbele zangu, na sote tusimame mbele za Kristo.

³⁹ Na kutoka kwenye kilindi cha moyo wangu, ninawaambia kutoka moyoni mwangu, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo, ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu, Naye alikufa na kufufuka tena, kisha akageuka akawa katika umbo la Roho, halafu akaja katika umbo la Roho Mtakatifu anayeishi Kanisani siku hizi, na anafanya na kutenda mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani, vivyo hivyo. Ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

40 Na si hilo tu, kama huu ndio wakati wa mwisho nitakaopata kushuhudia maishani mwangu, ushuhuda wangu ni wa kweli. Sisemi jambo hilo kwa nafsi yangu. Kama ningefanya hivyo, ningekuwa makosani. Sisemi lolote juu yangu mwenyewe ila ni mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Hivyo tu.

41 Mungu yeye yule aliyemponya Bartimayo kipofu, aliniponya. Yeye huwaponya wengine. Simponyi mtu yeyote. Siwezi kumponya mtu yeyote, bali Yeye huponya. Ameponya. Nao watu kwa imani hulikubali na wanaponywa.

42 Sasa, kama mtoto, Nuru hiyo ilitokea, nami sikujua ilikuwa ni nini. Ilionekana asubuhi ile ile niliyozaliwa na mama yangu. Loo, ninajua tuna mambo mengi sana, bali sizungumzii mambo mengine. Inanibidi tu kuwajibika kwa yaliyo yangu. Ndipo Hiyo—Hiyo ikaingia chumbani.

43 Kama mvulana mdogo, mwenye dhambi, ni—nilianza kuwaambia watu kuhusu kuiona Hii, wala watu hawakuamini; la hasha. Ndipo basi, wakaanza kuangalia jinsi ingetabiri mambo yatakayotukia, na kamwe hata wakati mmoja, nina umri wa miaka arobaini na sita, wala kamwe halijawahi kushindwa hata wakati mmoja, katika miaka hiyo, hata kidogo.

44 Nanyi mna gazeti, usiku wa leo, lenye unabii ulioandikwa tayari, kwamba, kile hasa kitakachotukia, limechapishwa. Angalieni mwone kama litatimia au la. Mnaona? Angalieni kama litatokea. Litatimia tu herufi kwa herufi jinsi linavyosema. Halijawahi kushindwa kamwe. Ni kitu gani? Si mimi, ni Yeye.

45 Halafu huko mtoni, wakati nilipowekwa wakfu kwa mara ya kwanza katika kanisa la Kibaptisti (mvulana wa miaka ishirini na mitatu, ama, mwanamume), Mungu alishuka siku hiyo nilipokuwa nikibatiza watu mia tano mtoni, ndipo akatokea katika Nuru iyo hiyo. Magazeti yaliandika makala yake. Halafu baadaye, wakasema, “Loo, vema, huenda ilikuwa ni saikolojia.”

46 Wakati inapoingia mikutanoni halafu watu, baadhi ya watu walio karibu sana na Mungu, ama, huenda ikawa sivyo, huenda ilikuwa ni kwa ajili yao. Watu wengine wanaweza kuona mambo na wengine hawaoni mambo.

47 Hakuna mtu aliyeona... Hakuna mtu katika, vituo vyote vya uchunguzi ambavyo ile Nyota kubwa ilipitia juu ya... Ni Wakristo wangapi wanaoamini kwamba kweli hao mamajusi waliifuata ile Nyota? Hebu tuone mkono wako. Historia hailinukuu popote, hakuna mahali pengine katika Biblia, mahali pengine popote, ila wale mamajusi, walipewa kuona Nyota hii, nao wakaweka wakati kwa nyota, na Hiyo ikapita na kusimama juu ya Yesu alipokuwa na umri wa miaka miwili.

48 Sasa, angalieni tena, wakati Paulo alipokuwa akienda zake Dameski kuwakamata hao watu, Nuru kuu ilimulika mbele zake angavu sana hata ikayapofusha macho yake. Nao watu waliosimama pale, hao askari na kadhalika karibu

naye, hawangeweza kuona Nuru yoyote. Hawakujua chochote kuhusu ile Nuru, lakini ilikuwa halisi sana kwa Paulo mpaka ikayapofusha macho yake; na wanadamu wengine wamesimama pale pale, wakiangalia na kufinya macho yao, wala hawangeweza kuona chochote. Mnaona?

Kwa hiyo, jukwaani ama popote pale, Yesu Kristo... Hiyo Nuru ilikuwa Nani? Yesu Kristo. “Ni nani Huyo ninayemtesa, Bwana?”

⁴⁹ Akasema, “Mimi, Yesu: na ni vigumu kwako kuupiga teke mchokoo.” Mnaona? Ilikuwa ni Yesu katika umbo la Nuru ambayo ilikuwa halisi sana kwa Paulo, ikayapofusha macho yake. Lakini watu waliosimama karibu hawangeweza kuona.

⁵⁰ Na mara nyingi, usiku baada ya usiku, kusema kweli, si sekunde mbili zilizopita, nilikuwa nikiangalia Kitu kile kile. Hiyo ni kweli. Wala haiko futi mbili kutoka mahali ninaposimama sasa hivi, ile ile. Lakini mnaona, iko katika kiwango kingine. Mnaona? Ni ninii... Ina—inapewa wengine, na halafu, na Mungu, katika upendo Wake na rehema, si kwa sababu yangu, maskini kiumbe kisichostahili (La, bwana.), bali kwa sababu ya Kanisa na hao watu, kwa sababu hamtakuwa na udhuru kwenye Siku ya Hukumu.

⁵¹ Lile Shirika kuu la Wapiga Picha la Marekani, baada ya magazeti mengi yaliyoipiga picha, waliipiga picha kwa kamera yao. Ndipo usiku mmoja huko Houston, Texas, Mungu akaruhusu picha Yake ya Mwanawe, katika umbo lile lile ambalo Mtakatifu Paulo alimwona, apate kupigwa picha. Nao wakamleta George J. Lacy wa alama ya vidole wa makachero wa FBI na hati kutoka California hadi Houston, Texas, kuiweka kwenye jengo la Shell, kwenye maabara, na kuichunguza chini ya miali ya nuru kali sana, na kadhalika, kwa siku baada ya siku. Ndipo akajitokeza (mkosoaji wangu mkali sana) na kunipa mkono na kusema, “Ndugu Branham, Nuru iligusa lenzi. Ilikuwapo.” Kisha kasema, “Jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia. Hiyo Nuru ilikuwako.”

⁵² Na kama nikifa usiku wa leo, ushuhuda wangu ni wa kweli: Mwana-kondoo yule yule wa Mungu aliyetolewa kwa ajili ya Bartimayo kipofu ametolewa kwa ajili ya kila kitu unachohitaji usiku wa leo, kama tu utaangalia na kuishi, ndugu yangu. Tazama uishi.

Twaweza kuomba?

⁵³ Mungu mpendwa, aliyemfufua Yesu tena katika wafu, akamfufua siku ya tatu, kwa sababu nabii Wako, Daudi, alisema ya kwamba Yeye hatakuwa mshiriki wa uharibifu, wala hutaiacha Nafsi Yake katika kuzimu, kwa hiyo Yeye alifufuka kabla ya mwili Wake kuharibika.

⁵⁴ Naye alisema, wakati alipokuwa hapa duniani, “Nilitoka kwa Mungu.” Hakika, Yeye alikuwa ile Nuru kuu ya Shekina

iliyokuwa pamoja na wale wana nyikani. Naye akasema, “Ninarudi kwa Mungu,” ile Nuru kuu ya Shekina iliyokutana na Paulo akienda zake Dameski.

⁵⁵ Na Wewe huyu hapa, leo, kwa uthibitisho usioweza kukosea, kwa vyombo vya kimitambo, kwa Ushuhuda wa Roho Mtakatifu, kwamba Wewe hujawaacha watu Wako, watu Wako ndio wamekuacha. Tunakuwa goigoi sana na kufungiwa hisi, mpaka tunategemea hisi zetu kwa mambo yote.

⁵⁶ Na Baba mpendwa, jalia kila mwanamume, mwanamke, mvulana, au msichana, hapa usiku wa leo, atoke kwenye hisia za hali hii ya duniani, aangalie huko ng'ambo Kalvari, na kujua ya kwamba Yesu, Mwana wa Mungu, ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁵⁷ Na, Baba Mungu, ninaomba ya kwamba utamtuma usiku wa leo, ile Shekina kuu. Jalia aje karibu sana na jengo hili hata hao watu wanaweza kujua Hiyo ndiyo inayozunguka humu jengoni. Hiyo ndiyo sababu roho zao zinasumbuka, hata wakati huu, ni kwa sababu Yeye yupo hapa. Basi jalia Uwepo Wake ulio mkuu sana umtie mafuta maskini mtu huyu, asiyestahili, usiku wa leo, kumthibitishia jamaa ambaye huenda akawa na shaka kidogo, ya kwamba Wewe upo hapa na unafanya mambo yale yale usiku wa leo pamoja na Kanisa Lako uliyofanya katika siku zilizopita pamoja na Mwanao, Kristo Yesu; kwa kuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

⁵⁸ Tusamehe dhambi zetu, Bwana, na utusaidie kuwa watumishi Wako. Wabariki watu hawa, wafanye wawe na moyo mnyenyekevu, na waipokee Injili. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao mpendwa. Amina.

[Dada mmoja ananena kwa lugha, kisha anafasiri—Mh.]
Haleluya!

Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yanawezekana, tu . . .

⁵⁹ Sasa, mwaminini kwa mioyo yenu yote sasa, enyi watoto. Basi chini ya tafsiri ya *dhambi*, inamaanisha “kutokuamini.” Kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Zingine zote . . . matendo haya ya utovu wa uadilifu ni matokeo tu ya hiyo moja: kutokuamini. “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Mnaona? Huna budi kuamini.

⁶⁰ Sasa, tutawaombea baadhi ya wagonjwa. Ninaamini walisema waligawa kadi za maombi. Ninaamini walikuwa na mia moja walizogawa, jana, za X, naamini. Kwa hiyo tunaanza . . . Hivi hatukuanza kutoka mia moja jana usiku? Hiyo si ilikuwa ni kweli? Tulienda kwenye mia moja, kisha tukarudi kinyumenyume. Sivyo? Au kitu fulani? Hebu tuanzia kwenye X, namba moja, halafu, usiku wa leo, kisha twende kufikia

yapata... Ni nani aliye na kadi ya maombi namba moja? X, namba moja? Namba...

Nakutakia heri, kipenzi. Msichana mdogo aliinua mkono wake. Mungu ambariki mtoto huyo mdogo.

Vema, namba moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Hebu hao wasimame kwanza, tafadhalini.

Na kama mpiga piano atapiga, ama, mpiga kinanda (Samahani, dada.), *Amini Tu* tena, sivyo?

⁶¹ X, namba moja hadi—hadi kumi. Ni wangapi, wakati hawa wakichukua mahali pao... Kama huwezi kusimama, sasa, kama namba yako imeitwa, wala huwezi kusimama, inua tu mkono wako. Mabawabu watakubeba wakati namba yako itakapoitwa. X, moja hadi kumi.

⁶² Sasa, ni wangapi hapa ndani, sasa hivi, wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, mimi... Mnaamini Huyu ni Roho Mtakatifu? Hakika. Kuna rafiki mwenye dhambi hapa ndani angesema, kwa hili, “Mungu, mimi ni mwenye dhambi na ninataka Wewe unikumbuke sasa”? Mimi—mimi, hatutawaita madhabahuni. Huduma za madhabahuni ni nzuri. Tunaziamini. Lakini hata hivyo, Biblia ilisema, “Wote walioamini waliongezwa kwa Kanisa.”

⁶³ Utainua mkono wako? Useme, “Nikumbuke, Mungu.” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, mama. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, mama. Hilo ni sawa. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, na wewe, na wewe. Hilo ni sawa.

⁶⁴ Katika roshani huko juu, mtu fulani aseme, “Mungu nikumbuke. Ni—ninataka kuja Kwako kwa amani siku moja.” Mungu akubariki, bwana. Hilo ni sawa. “Ninataka kukumbukwa katika maombi, Ndugu Branham. Nami na—nakutaka uniombee. Ninamwinulia Mungu mkono wangu.” Lifanye sasa hivi. Ungelifanya? Mtu mwingine? Tunapongojea, vema, mtu mwingine utainua mkono wako? Sema, “Nikumbuke.” Mtu fulani bado hajainua mkono wake. Mungu akubariki, mama. Bwana na atujalie hilo. Vema.

Sasa hebu tuwaombe.

⁶⁵ Baba wa Mbinguni, jalia kila mtu aliyeinua mkono wake sasa hivi... Kitu fulani kiliugusa moyo wao. Wanajua wako katika Uwepo wa Kiungu, ingawa huenda wasiweze kuliona jinsi tunavyoliona sasa, katika Utukufu huu mkuu wa Shekina. Lakini wao, kuna kitu fulani kuhusu nafsi yao ya kibinadamu kinachohisi Hilo. Wanajua kuna kitu Fulani mahali fulani. Hawajui ni wapi hasa, bali wanajua ya kwamba kitu Fulani kimevagusa kiajabu.

⁶⁶ Hebu na tulisikilize Neno la Mungu: lililosema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu.” Kwa

hiyo, Bwana, jalia watambue ya kwamba hawapo mahali popote tofauti na kuketi Uweponi mwa Bwana Yesu. Roho Wake yuko hapa. Ule Utukufu mkuu wa Shekina sasa uko hekaluni usiku wa leo.

Nami naomba, Baba, ya kwamba Wewe utawaokoa. Jalia walikubali sasa hivi miyoni mwao. Kwa kuwa tunaomba katika ninii Yake. . . Jina la Yesu. Amina.

⁶⁷ Vema, tuna. . . Hao walikuwa wangapi? Kumi? Vema, sasa, kumi hadi kumi na tano simameni. X, kumi hadi kumi na tano ingieni mstarini moja kwa moja. Sasa, tuna nafasi zaidi kule, ndugu? Tuna nafasi zaidi. Ni nani aliye na X, kumi na moja? Hebu tuone mkono wako. Njoo huku, ukiweza. Kumi na moja? Vema, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

⁶⁸ Haijalishi ni wangapi wanaosimama, lakini hatutaki kila mtu kusimama ikubidi kuwa unangojea. Nasi hatuna budi kuwa na utaratibu wake wa namna fulani kwa sababu usipofanya hivyo, kuna msongamano tu hapa jukwaani, wala huwezi kupata utaratibu kwa ajili ya chochote.

⁶⁹ Sasa polepole, wakati wakichukua nafasi zao, hebu na tuimbe kwa upole sasa. Mnaupenda wimbo huo, *Amini Tu?* Mwajua, niliusikia ukiimbwa katika lugha ishirini na kitu mbalimbali, ukinihalika jukwaani. Na siku moja, kama Yesu akinichukua kabla hajaja dhahiri katika mwili wa nyama kulipokea Kanisa Lake, na inibidi kuzikwa, na iwe ni kura yangu kuingia kwenye mavumbi ya ardhi, kama punje ya mahindi, ni—nimepanga: watauimba huo watakapokuwa wakinishusha kaburini. Ukisikia habari zangu, kwamba, nimewaacha, wewe simama kwa dakika chache tu, kidogo uuvumishe huo mwenyewe, na kusema, “Utukufuni, angali anaamini.” Ninaamini. Ninaamini. Mnafikiri nitafahamu hayo? Hakika. Bila shaka, nitafahamu.

⁷⁰ Samueli, baada ya kufa kwa muda mrefu, huyo hapo amesimama; angali alikuwa ni nabii, pia. Alikuwa amevaa joho lake la nabii. Maskini yule mchawi, aliyekuwa amemwita kutoka Paradiso, alimwangukia, kasema, “Naona miungu ikizuka.” Si kwamba tu alikuwa amevaa mavazi yake ya nabii, bali alikuwa angali ni nabii. Aliwaambia yale yaliyokuwa yanaenda kutukia kesho yake, na ikawa hivyo.

⁷¹ Hakika, hatufi. Tunakufa sisi kwa sisi, bali tungali Uweponi mwa Mungu. Amina. Yesu hajafa. Naye alisema, “Kwa kuwa Mimi ni hai, ninyi nanyi mtaishi pia.” Hilo liko moyoni mwangu, limetulia tu hapo Milele, nami ninaliamini. Nami ninajua ya kwamba Yeye yupo hapa usiku wa leo. Nami ninajua ya kwamba Yeye hufanya mambo yote, na anayafanya vizuri.

⁷² Sasa, marafiki, wakati Billy alipokuja na kunichukua usiku wa leo, alisema, barabarani tukija, alisema, “Baba,” kasema,

“unawachelewesha watu mno.” Nami nimeona nimechelewa sana. Samahani. Na tukijua ya kwamba kila kitu kitakuwa jinsi kilivyo, ni saa nne na robo sasa, yapata dakika kumi na saba baadaye kwa saa ya ukutani pale.

⁷³ Laiti mngenipa fadhili usiku wa leo. Je, mtanipa? Sasa, kwa ajili tu ya Injili: kama mtaketi tu kimya kwa muda kidogo tu; msiwe mkizunguka-zunguka. Tulieni tu kabisa. Na labda kama huamini jambo hilo, ninii tu—ninii tu... usininii... keti tu kimya, useme, “Vema, nita—nitamwomba Mungu, ‘Kama ni kweli, anijulishe.’”

⁷⁴ Sasa, kuna watu wengi hapa ambao ni wagonjwa; labda wengi ambao hata hawana kadi za maombi, lakini Yesu Kristo anajua yote kuwahusu. Mnaamini hilo? Hakika. Anaweza kukupa afya. Amini sasa. Ni wangapi wasio na kadi za maombi na wanataka kuponywa? Hebu tuone mkono wako. Sijali uko wapi. Mnaona. Vema, hiyo ni... .

⁷⁵ Sasa, mguse tu kama yule mwanamke alivyomgusa. Unaona? Mguse tu, useme (Yeye ni Kuhani Mkuu), “Sasa, Bwana, si—sitegemei viwango hivi vitatu ninamoishi; ninaenda Kwako, kwa imani, naja. Nitakuomba, sasa, unirehemu na unijalie uponyaji wangu.” Naye atafanya hivyo. Yeye aliyeahidi ni mwaminifu. Hivi hamwamini hilo? Bila shaka ndivyo alivyo.

⁷⁶ Sasa iweni tu watulivu na wenye kicho. Na sasa, ninataka kuweka hili kwa watu, wakati, nafikiri, wangali wanapanga baadhi ya mstari wa maombi kule. Ninataka kuwapa watu jambo hili: Kama Yesu Kristo amefufuka katika wafu, basi atakuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na sasa, ninaamini, kama Mkristo, kwamba Yeye amekuwa, na sasa yuko, kama tu alivyokuwa katika siku zilizopita wakati alipokuwa hapa katika mwili; ila tu Yeye yupo hapa katika umbo la Roho, akifanya kazi kupitia watu binafsi ambao Yeye, kwa kutangulia kujua kwa Mungu kabla ulimwengu haujaumbwa, Yeye alijua ya kwamba watu hawa wangekuwako duniani. Unaamini hilo? Hiyo ni Biblia.

⁷⁷ Wewe si kitu fulani ati kwa sababu unatamani kuwa kitu fulani; wewe ni kitu fulani, uko jinsi ulivyo, kwa mapenzi ya Mungu. Unaona? “Mungu ameweka Kanisani.” Unaona? Unaona? Usiingie katika mwili, kamwe haitafaulu. Kaa mahali Mungu anapokuweka. Unaona? Ni kwa... . “Karama na miito havina majuto.” Vimejulikana na Mungu tangu zamani. Mungu haninii... Yeye hakuweka tu sheria iliyokazwa kwa chuma kwamba ungefanya ama usingefanya; bali kujua Kwake tangu zamani kulimfanya aweze kuchagua tangu zamani kwa kujua tangu zamani. Kuchaguliwa tangu zamani huangalia nyuma kwenye kujua tangu zamani, kujua tangu zamani huangalia hatima.

⁷⁸ Lakini Yeye yupo hapa, Naye yupo hapa usiku wa leo. Na kama atajithibitisha kuwa hai pamoja nanyi usiku wa leo katika miujiza, mambo ya kimbinguni, kama tu alivyofanya hapa duniani, hivi kila mtu humu ndani atamwamini kwa moyo wako wote? Utafanya hivyo? Basi ombeni, na mniombee.

Sasa, mnatambua yale... Nimesimama hapa. Kuna mtu angetaka kuchukua mahali pangu? Nitafurahi kama... kuja huku kuwaombea wagonjwa. Mnaona?

⁷⁹ Sasa, ni changamoto. Ni changamoto kwenu. Nami sisemi ya kwamba Roho Mtakatifu atafanya hivyo. Sijui. Ni juu Yake. Mimi ni mtumishi Wake tu.

⁸⁰ Sasa, mstari wa maombi uko tayari? Vema, nani? Huyu ndiye wa kwanza, ama, huyu ndiye mama wa kwanza? Vema, unaangalia? Vema, bwana. Njoo hapa, mama.

Sasa, kama utampa Bwana Yesu usikivu wako mkamilifu. Sasa, fungia tu mbali mashaka yote kutoka moyoni mwako.

⁸¹ Musa, yule nabii, alipewa ishara mbili za kufanya mbele ya wana wa Israeli. Alizifanya wakati mmoja nao Israeli wote wakamfuata hadi kwenye nchi ya ahadi.

⁸² Kama Yesu anaweza kuthibitishwa usiku wa leo kuwa yu hai, na njia pekee... Inawezekana mtu aje hapa akiwa na makovu mikononi mwake; huyo angeweza kuwa ni mnafiki. Mnaona? Hilo linaweza kuwa ni kitu chochote kidanganyifu. Ibilisi angeweza kujitokeza namna hiyo. Lakini Yesu akitokea, Yeye atatokea kwa njia ile ile aliyosema angetokea, si chochote kinyume. Kwa hiyo, kama Yesu atajitokeza hapa usiku wa leo na kufanya mambo ambayo alisema angefanya, basi wewe mwamini kwa moyo wako wote.

Sasa, nadhani huyu mama hapa mbele yangu, nadhani hatufahamiani, siyoy, mama? Vema.

⁸³ Sasa, mama huyu aliyesimama hapa, ninii tu, ndiye mtu wa kwanza. Sababu ya mimi kumleta na kumweka hapa, nje peke yangu, ni kwanza, ule upako. Unajua ya kwamba kitu Fulani kipo hapa. Sasa, hatutaharakisha. Chukua wakati wako. Nasi tunaninii... Iweni na kicho.

⁸⁴ Na sasa, tunajua ya kwamba Kitu fulani kipo hapa. Sasa, hebu tuone kile Biblia ilichosema. Biblia ilisema, "Iwapo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao. Nitakuwa katikati yao, daima, sikuzote, hata mwisho wa ulimwengu, nitakuwa pamoja nao. Na mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya, pia."

⁸⁵ Sasa, huyu hapa mwanamke, kama tu ilivyokuwa na Bwana wetu akisimama kisimani; mimi ni mwanamume, yeye ni mwanamke. Yeye alikuwa Mwanamume; yule mwanamke kisimani, alikuwa ni mama Msamaria. Sasa, simjui mwanamke *huyu*, Yeye hakumjua mwanamke *huyu*; bali alianza

kuzungumza naye. Na wakati Yeye—Yeye alipozungumza naye, vema, alipata kujua mahali shida yake ilipokuwa. Naye akamwambia mahali shida yake ilipokuwa nalo li—likamsisimua sana, mpaka akakimbilia mjini na—na akaanza kusema, “Njoni, mwone Mtu.” Hiyo ni kweli. Si ni kweli, kama wasomaji wa Biblia ya Kikristo? Yohana Mtakatifu 4.

⁸⁶ Nathanaeli alimjia, naye akasimama, Naye akamwambia Nathanaeli mahali alipokuwa, jambo fulani alilofanya kabla hajaja, na kumwambia alikuwa ni mwaminio. Nathanaeli akasema, “Wewe ni Mwana wa Mungu.” Na mengi, mengi, mengi, mengi, naam, moja kwa moja chini, chini, yalitendeka.

⁸⁷ Sasa kama ni Kristo, Yeye anaweza kufanya jambo lile lile, kama ninaweza kujitolea kwa Roho Wake. Unaweza kujitolea kwa Roho Wake; uanze kupaza sauti. Mtu mwingine huenda akasalimisha roho yao, na kuanza kuhubiri. Lakini ninapoitoa roho yangu, maono hutokea, maana nilizaliwa kwa ajili ya jambo hilo. Mnaona?

⁸⁸ Sasa, kama ninaweza kujitolea kwa Roho Mtakatifu aliyebarikiwa, Naye anaweza kuniambia kile dada yetu, shida yake ni nini, ama kilichomleta hapa, ama jambo fulani kulihusu, ambalo unajua silijui. . .Ningekujua? Tulizaliwa, labda, umbali wa maili nyingi, na kuachana kwa miaka mingi, na ndiyo mara ya kwanza maishani tumewahi kukutana. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

⁸⁹ Sasa, je, watu wanaona? Sijui lolote kumhusu mwanamke huyo hata kidogo. Mungu anajua hilo. Lakini kama Yeye anaweza, kwa Roho Wake Mtakatifu, kunijalia nijue. . .Vema, yeye yupo hapa kwa kusudi fulani: labda yeye ni mgonjwa, labda si mgonjwa; labda ana shida; labda amesimama hapo kwa ajili ya mtu mwingine. Sijui. Mnaona? Yeye hufanya hivyo. Lakini kama Yeye ataniambia jambo fulani kumhusu, mtakubali, basi, kwamba hiyo ni. . .Ama tuseme kwamba Yeye angeniambia kilichokuleta hapa, basi utakubali, huku Yeye, ukiwazia, ukiamini na kujua ya kwamba Yeye yupo hapa kukupa wewe. Hiyo ni kweli? Je, kusanyiko lote litaamini ya kwamba Yeye angewafanyia jambo lile lile? 

55-0400 Bartimayo Kipofu
Unknown
Alberta Canada

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org